# HALMASHAURI YA KIJIJI CHA NANJIRINJI A

# MPANGO WA UVUNAJI

## Mbumbila A

**March 2018 – February 2022**

# 1: MAANA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

**CBH** Mzunguko katika kimo cha kifua

**MD** Miti Midogo – ilionyeshwa kama miti myekundu wakati wa uhesabuji.

**KT** Miti ya Kati – ilionyeshwa kama miti ya kijani wakati wa uhesabuji.

**MK** Miti Mikubwa – ilionyeshwa kama miti ya bluu wakati wa uhesabuji.

**MT** Jumla ya umbali wa matembezi ya kukatisha msitu

**EK** Eneo la kuvuna

**NK** Namba ya kuzidisha eneo ili kupata makadirio

**cm** Sentimeta

**km** Kilometa

**ha** Hektari

**$m^3$** Mita za ujazo

# 2: MUHTASARI

Mpango huu utatekelezwa kulingana na maelekezo ya mpango wa usimamizi Misitu ulioandaliwa na kamati ya Maliasili ya Kijiji cha Nanjirinji A chini ya uwezeshaji wa Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Maendeleo (MCDI) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, na hatimaye kupitishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa mnamo Agosti 2016. Mpango huu unatoa mwongozo wa uvunaji endelevu katika Msitu wa Kijiji cha Nanjirinji A unaoitwa Mbumbila A.

Uvunaji utafanyika kipindi cha kiangazi, kinachoanza Mwezi wa Sita (Juni) mpaka mwanzoni mwa mwezi wa kumi na mbili (Desemba) kwa kuwa katika kipindi cha masika kunakuwa na uharibifu kama vile mmomonyoko wa Ardhi.

| | |
|---|---|
| Jumla ya Eneo la Msitu | 64,617 ha |
| Eneo lililotengwa kwa ajili ya Uhifadhi (Hakuna uvunaji) | 51,475 ha |
| Eneo la kuvuna | 13,142 ha |
| Aina ya Uoto | Miombo / Msitu ya Ukanda wa Pwani |
| Aina ya Miti | Mpingo *(Dalbergia melanoxylon),* Mninga Jangwa *(Pterocarpus angolensis),* Mpangapanga *(Millettia stuhlmannii), Mlondondo (Xeoderis stuhlmannii), Mninga bonde (Pterocarpus holtzii),* Msufi Pori *(Bombax rhodognaphalon),* Mkongo *(Afzelia quanzensis),* Mgongo, Mchenga (*Brachystegia speciformis),* Mkwaju, Mlipa deni, Msenjele, Mnidu, Mkwaju, Mpupi na Mkunya. |
| Mmiliki | Nanjirinji A |
| Meneja/Msimamizi | Kamati ya Maliasili, Nanjirinji A. |
| Aina ya Usimamizi | Usimamizi Shirikishi misitu ngazi ya Jamii unaofuata kanuni za uthibitishwaji wa Misitu. |
| Kiwango cha uvunaji | Cha chini |
| Kiwango cha Juu cha uvunaji kwa mwaka | **1209.06** mita za ujazo |

Kulingana na zoezi la uhesabuji wa mazao ya kuvuna ndani ya Msitu lililofanyika kati ya tarehe 11/2/2018 na tarehe 21/2/2018 Mti ulioonekana kwa wingi na tayari kuvunwa ni Mti Mpingo *(Dalbergia melanoxylon),* Mninga Jangwa *(Pterocarpus angolensis),* Mpangapanga *(Millettia stuhlmannii), Mlondondo (Xeoderis stuhlmannii), Mninga bonde (Pterocarpus holtzii),* Msufi Pori *(Bombax rhodognaphalon),* Mkongo *(Afzelia quanzensis),* Mgongo, Mchenga (*Brachystegia speciformis),* Mkwaju, Mlipa deni, Msenjele, Mnidu, Mkwaju, Mpupi na Mkunya.

Jedwali lililopo hapo chini lina ainisha kiasi endelevu kwa kila daraja la Miti kulingana na ukubwa itakayovunwa kwa kipindi cha miaka mitano cha mpango huu wa uvunaji. Namna ambavyo kiasi cha uvunaji kilipatikana imeelezwa katika sehemu ya nane ya mpango huu. Mabaki ya Miti iliyovunwa ambayo yaliachwa na mteja yatakuwa mali ya Kijiji na yatauzwa kwa mteja mwingine atakapopatikana kwa bei elekezi ya Serikali.

| Daraja la Miti | Ukubwa wa Miti | Vipimo Mzunguko (CBH) | Kiasi kwa miaka 5 |
|---|---|---|---|
| Mpingo | Miti ya Kati (KT) | 76 – 151 cm | 9.17 |
| Mpingo | Miti miKubwa (MK) | 152 cm au Zaidi | 3.95 |
| Mpangapanga | Miti ya Kati (KT) | 173 – 345 cm | 7.95 |
| Mpangapanga | Miti miKubwa (MK) | 346 cm au Zaidi | 0 |
| Msenjele | Miti ya Kati (KT) | 126 – 251 cm | 24.62 |
| Msenjele | Miti miKubwa (MK) | 252 cm au Zaidi | 0.69 |
| Mlondondo | Miti ya Kati (KT) | 142 – 283 cm | 15.43 |
| Mlondondo | Miti miKubwa (MK) | 284 cm au Zaidi | 0 |
| Mninga jangwa | Miti ya Kati (KT) | 142 – 283 cm | 4.26 |
| Mninga jangwa | Miti miKubwa (MK) | 284 cm au Zaidi | 0 |
| Mkongo | Miti ya Kati (KT) | 173 – 345 cm | 2.23 |
| Mkongo | Miti miKubwa (MK) | 346 cm au Zaidi | 0 |
| Mkwaju | Miti ya Kati (KT) | 173 – 345 cm | 6.31 |
| Mkwaju | Miti miKubwa (MK) | 346 cm au Zaidi | 0 |
| Mgongo | Miti ya Kati (KT) | 173 – 345 cm | 8.78 |
| Mgongo | Miti miKubwa (MK) | 346 cm au Zaidi | 0 |
| Mpupi | Miti ya Kati (KT) | 173 – 345 cm | 1.83 |
| Mpupi | Miti miKubwa (MK) | 346 cm au Zaidi | 0 |
| Msufi Pori | Miti ya Kati (KT) | 173 – 345 cm | 2.64 |
| Msufi Pori | Miti miKubwa (MK) | 346 cm au Zaidi | 0 |
| Mchenga | Miti ya Kati (KT) | 142 – 283 cm | 3.04 |
| Mchenga | Miti miKubwa (MK) | 284 cm au Zaidi | 0 |
| Mnidu | Miti ya Kati (KT) | 173 – 345 cm | 1.44 |
| Mnidu | Miti miKubwa (MK) | 346 cm au Zaidi | 0 |
| Mkunya | Miti ya Kati (KT) | 173 – 345 cm | 4.67 |
| Mkunya | Miti miKubwa (MK) | 346 cm au Zaidi | 0.31 |
| Mninga bonde | Miti ya Kati (KT) | 142 – 283 cm | 0.81 |
| Mninga bonde | Miti miKubwa (MK) | 284 cm au Zaidi | 0.31 |
| Mnepa | Miti ya Kati (KT) | 173 – 345 cm | 0.81 |
| Mnepa | Miti miKubwa (MK) | 346 cm au Zaidi | 0 |
| Mlipa deni | Miti ya Kati (KT) | 142 – 283 cm | 1.83 |
| Mlipa deni | Miti miKubwa (MK) | 284 cm au Zaidi | 0 |
| Mtumbitumbi | Miti ya Kati (KT) | 173 – 345 cm | 0.43 |
| Mtumbitumbi | Miti miKubwa (MK) | 346 cm au Zaidi | 0 |

# 3: UTANGULIZI

Ni muhimu Kamati ya Maliasili kutekeleza mpango wa uvunaji kama ilivyoainishwa katika mpango wa usimamizi misitu. Kama miti mingi itavunwa kupita kiwango kilichoainishwa ndani ya mpango huu basi msitu utakuwa umeelekezwa katika mpango ambao si wa uvunaji endelevu na Mkurugenzi wa Misitu anaweza kusitisha kutambua hadhi ya msitu huo. Kuepusha matatizo kama hayo yasitokee kamati za maliasili zinashauriwa kuelewa vyema mpango wa usimamizi misitu. Kila aina ya mti itakuwa na mpango wake wa uvunaji. Kama

kutakuwa na utata juu ya namna hatua za uvunaji zitakavyofanyika kamati ya maliasili itawasiliana na Afisa misitu wa Wilaya au Mradi wa Kuhifadhi Mpingo ili kupata ushauri.

## 4: MADHUMUNI YA MPANGO WA UVUNAJI

Ili kupunguza madhara ya kimazingira na gharma za usimamizi uvunaji utafanyika kwa kiwango cha chini kwa kutokuzidisha 20% ya kiwango cha kuvuna kwa mwaka. Kutoa mwongozo unaozingatia uvunaji endelevu wa miti ya Mpingo *(Dalbergia melanoxylon),* Mninga Jangwa *(Pterocarpus angolensis),* Mpangapanga *(Millettia stuhlmannii), Mlondondo (Xeoderis stuhlmannii), Mninga bonde (Pterocarpus holtzii),* Msufi Pori *(Bombax rhodognaphalon),* Mkongo *(Afzelia quanzensis),* Mgongo, Mchenga (*Brachystegia speciformis),* Mkwaju, Mlipa deni, Msenjele, Mnidu, Mkwaju, Mpupi na Mkunya. katika msitu wa kijiji cha Nanjirinji A.

- Mpingo (*Dalbergia melanoxylon*) – Mzungukokatika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 76.
- Mlondondo*(Xeoderis stuhlmannii)* - Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 142
- Mninga jangwa*(Pterocarpus angolensis)* - Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni Sentimita 142
- Mpangapanga(*Millettia stuhlmannii*) - Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173
- Mgelegele- Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173
- Mkongo(*Afzelia quanzensis)* - Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173.
- Mninga bonde(*Pterocarpus holtzii*) – Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 142
- Msufi pori (*Bombax rhodognaphalon*) – Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173.
- Mgongo – mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173.
- Mchenga (*Brachystegia speciformis*) – Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni Sentimita 142.
- Mkwaju - Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173.
- Mlipa deni - Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173.
- Msenjele - Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173.
- Mnidu - Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173.
- Mkwaju - Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173.
- Mpupi - Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173.
- Mkunya- Mzunguko katika kimo cha kifua unaoruhusiwa kisheria ni sentimita 173.

Kutoa mwongozo unaozingatia uvunaji endelevu wa Miti

Mwongozo huu utahusu aina ya Mti mmoja tu, na unatoa kiasi cha uvunaji endelevu kwa kila Mti husika. Jamii ya Miti ambayo haijatajwa hapo juu itavunwa kwa kufuata mpango wa uvunaji mwingine au kutovunwa kabisa.

## 5: TANGAZO LA KUVUNA

Maelezo ya maombi yaliyopitishwa ya uvunaji wa Miti toka kwenye Msitu wa Kijiji uliothibitishwa na unaosimamiwa na kamati ya Maliasili au kamati iliyopewa jukumu kama hilo ni lazima yabandikwe kwenye mbao za Matangazo za Kijiji siku mbili kabla ya kuanza uvunaji, tangazo hili litakuwa na maelezo yafuatayo:

a) Jina la Mwombaji (Jina la kampuni na wawakilishi).
b) Siku maombi yalipopokelewa, yalipopitishwa na lini uvunaji unategemewa kuanza.
c) Aina ya Miti na kiasi cha miti alichokubaliwa kuvuna mteja (makadirio ya idadi ya magogo na idadi ya magari yatakayobeba mzigo).
d) Mapato yanayotegemewa kutokana na uvunaji huo au kiasi cha pesa zilizolipwa hapo Kijijini.
e) Mapato kamili yaliyopatikana kutokana na uvunaji (sehemu hii ijazwe baada ya uvunaji kufanyika).
f) Jina la eneo uvunaji utakapofanyika ndani ya Msitu wa hifadhi.

## 6: MAENEO YA UVUNAJI

Uvunaji hautaruhusiwa katika maeneo yafuatayo;

- Katika kingo za mito umbali wa mita Sitini kutoka katikati ya mito ya kudumu inayotiririsha maji mwaka mzima au vyanzo vya maji vya kudumu (visivyokauka mwaka mzima).
- Eneo ndani ya mita 20m toka vijito au kingo za mito au mita 30 toka kingo za mito midogo kama ilivyobainishwa katika Mpango wa Usimamizi.
- Ndani ya eneo ambalo umbali toka kingo za vijito vya muda vilivyosababishwa na mvua za masika ni sawa na upana wa vijito hivyo. Kwa mfano katika eneo la Mita 2 toka kingo za Kijito chenye upana wa Mita 2.
- Katika miteremko mikali (kupunguza mmomonyoko wa udongo). Maeneo haya yameainishwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 sehemu ya III kama maeneo yanayoweza kuathirika zaidi.
- Maeneo yanayojulikana kuwa na umuhimu kwa Jamii kwa shughuli za kijadi na kimila kama vile kutambikia na kuabudia.
- Maeneo yanayohifadhi Maji kwa muda mfupi au kwa kudumu yanayotumiwa na wanyamapori.
- Maeneo yaliyo karibu na vyanzo vya maji.

## 7: UKATAJI WA MITI

Uvunaji holela unaweza ukaathiri uvunaji endelevu. Kama taarifa za uvunaji holela hazikutolewa kwa mradi wa kuhifadhi mpingo, kiwango kilichovunwa kiholela kitapunguzwa kwenye mgawo utakaofuata/salio la mgawo uliobakia.

Utengenezaji barabara au njia ndani ya msitu wa hifadhi ni lazima upate idhini ya Halmashauri ya Wilaya. Na ni lazima uzingatie kupunguza uharibifu wa miti mingine na athari za kimazingira.

Uvunaji hautafanyika katika eneo moja ndani ya msitu bali katika maeneo tofauti kwa kuchagua miti iliyo komaa. Ili kurahisisha utoaji wa magogo msituni, eneo la uvunaji ni sharti likachaguliwa kwa uangalifu ili kuzuia adhari kwa miti na mimea mingine. Mwelekeo wa kutolea magogo pia ni vyema ukazingatiwa ili kupunguza athari kwa miti mingine.

## 8: USIMAMIZI NA USALAMA KATIKA KUVUNA

Uvunaji hautarusiwa kufanyika ndani ya eneo la Msitu bila usimamizi wa Umoja wa Wavuna Mbao Lindi (UWAMBALI) au mtaalamu yeyote atakayekuwa amechaguliwa na Afisa Misitu Wilaya kusimamia kazi hiyo. Utaratibu mzuri wakati wa kuvuna ni muhimu kwa usalama wa wavunaji na hupunguza athari kwa miti mingine.

Tahadhari muhimu za kiusalama wakati wa kuvuna ni pamoja na:

- Vitendea kazi vya kujikinga na athari za uvunaji ni lazima vitolewe kwa wavunaji wakati wa kuvuna kama vile viatu vya buti, kofia za kuvunia miti,vifaa vya kuzuia vumbi puani na glovu za kuvaa mikononi.
- Sanduku la huduma ya kwanza ni lazima liwepo katika shughuli zote za uvunaji.
- Misumeno na mashoka ya kukatia iwe na makali ya kutosha.
- Taratibu za uvunaji ni lazima zizingatie kupunguza mabaki ya miti au kupoteza sehemu kubwa ya miti.
- Ni marufuku kutumia mashine ya nyororo (chain saw) kweye Msitu wa Kijiji.
- Mbinu za kuangusha miti ni lazima zizingatie mwelekeo wa Mti.
- Uvutaji sigara hauruhusiwi ndani ya Msitu.
- Hairuhusiwi kuwasha moto Msituni.
- Matenki ya kuhifadhia mafuta kwa ajili ya magari na matrekta hayaruhusiwi kuwepo msituni.

## 9: MISITU ENDELEVU

Msitu endelevu ni Msitu unaosimamiwa vizuri na unaoweza kukidhi mahitaji ya sasa na ya vizazi vijavyo bila matatizo. Malengo hayo yanaweza kufikiwa kwa kuhakikisha kuwepo kwa uwiano mzuri kati ya miti inayokatwa na kiasi cha miti iliyopo na ukuaji wa miti hiyo. Kiasi cha miti inayovunwa haitakiwi kuzidi kiwango cha ukuaji wa Miti mingine. Pia ni lazima kuzingatia kiasi cha Miti itakayokufa kwa kuathirika na magonjwa mbalimbali na mabadiliko ya Asili.

## 10: MGAO WA UVUNAJI

Jedwali hapo chini linaonyesha jamii za miti, mzunguko katika kimo cha kifua, madaraja matatu wakati wa kuvuna na kiasi cha kuvunwa kiendelevu kwa kipindi cha miaka mitano

cha mpango huu wa uvunaji. Miti ya daraja la miti midogo (MD) hairuhusiwi kuvunwa kisheria.

| **Jamii** | **Daraja** | **Mzunguko kimo cha kifua (CBH)** | **Kiasi cha kuvuna kwa kipindi cha miaka mitano** |
|---|---|---|---|
| Mpingo | MD | 38 – 75 cm | 0 |
| Mpingo | KT | 76 – 151 cm | 9.17 |
| Mpingo | MK | 152+ cm | 3.95 |
| Mpangapanga | MD | 87 – 172 cm | 0 |
| Mpangapanga | KT | 173 – 345 cm | 7.95 |
| Mpangapanga | MK | 346+ cm | 0 |
| Msenjele | MD | 63 – 125 cm | 0 |
| Msenjele | KT | 126 – 251 cm | 24.62 |
| Msenjele | MK | 252+ cm | 0.69 |
| Mlondondo | MD | 71 – 141 cm | 0 |
| Mlondondo | KT | 142 – 283 cm | 15.43 |
| Mlondondo | MK | 284+ cm | 0 |
| Mninga jangwa | MD | 71 – 141 cm | 0 |
| Mninga jangwa | KT | 142 – 283 cm | 4.26 |
| Mninga jangwa | MK | 284+ cm | 0 |
| Mkongo | MD | 87 – 172 cm | 0 |
| Mkongo | KT | 173 – 345 cm | 2.23 |
| Mkongo | MK | 346+ cm | 0 |
| Mkwaju | MD | 87 – 172 cm | 0 |
| Mkwaju | KT | 173 – 345 cm | 6.31 |
| Mkwaju | MK | 346+ cm | 0 |
| Mgongo | MD | 87 – 172 cm | 0 |
| Mgongo | KT | 173 – 345 cm | 8.78 |
| Mgongo | MK | 346+ cm | 0 |
| Mpupi | MD | 87 – 172 cm | 0 |
| Mpupi | KT | 173 – 345 cm | 1.83 |
| Mpupi | MK | 346+ cm | 0 |
| Msufi Pori | MD | 87 – 172 cm | 0 |
| Msufi Pori | KT | 173 – 345 cm | 2.64 |
| Msufi Pori | MK | 346+ cm | 0 |
| Mchenga | MD | 71 – 141 cm | 0 |
| Mchenga | KT | 142 – 283 cm | 3.04 |
| Mchenga | MK | 284+ cm | 0 |
| Mnidu | MD | 87 – 172 cm | 0 |
| Mnidu | KT | 173 – 345 cm | 1.44 |
| Mnidu | MK | 346+ cm | 0 |
| Mkunya | MD | 87 – 172 cm | 0 |
| Mkunya | KT | 173 – 345 cm | 4.67 |
| Mkunya | MK | 346+ cm | 0.31 |
| Mninga bonde | MD | 71 – 141 cm | 0 |
| Mninga bonde | KT | 142 – 283 cm | 0.81 |
| Mninga bonde | MK | 284+ cm | 0.31 |
| Mnepa | MD | 87 – 172 cm | 0 |
| Mnepa | KT | 173 – 345 cm | 0.81 |
| Mnepa | MK | 346+ cm | 0 |
| Mlipa deni | MD | 71 – 141 cm | 0 |
| Mlipa deni | KT | 142 – 283 cm | 1.83 |
| Mlipa deni | MK | 284+ cm | 0 |
| Mtumbitumbi | MD | 87 – 172 cm | 0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mtumbitumbi | KT | 173 – 345 cm | 0.43 |
| Mtumbitumbi | MK | 346+ cm | 0 |

## 11: KIWANGO CHA CHINI CHA UVUNAJI MAGOGO

Kiwango cha chini cha uvunaji wa magogo ni uvunaji wa mbao ambazo kiwango hakitazidi 20% ya wastani wa ongezeko la mwaka la ujazo wa Mti katika Msitu, na kiwango cha juu cha 5,000$m^3$ kwa mwaka. Wastani wa ongezeko la mwaka, ni wastani wa ujazo wa Mti ambao unategemewa kuongezeka kila mwaka, na unakokotolewa kwa kila Jamii ya Miti na sio kwa hiyo iliyo tajwa hapo juu kwa uvunaji. Mahesabu yafuatayo yanaelezea kiwango cha mbao ambacho kinatakiwa kuvunwa kwa mwaka ilikuweza kubaki katika kiwango cha chini. Ina kokotolewa kutoka kwenye takwimu ya mistari ya utafiti ya kudumu inavyotumika katika ufuatilaji wa hali ya msitu (inayohusisha jamii yote ya miti), na sio matembezi ya kukatisha msitu yanayotumika katika tathimini ya kupata kiasi cha mgao wa uvunaji.

| | |
|---|---|
| Eneo la Msitu Kuvuna (EK) | **13,142** |
| Wastani wa Ongezeko la Mwaka (WOM) | **0.46$m^3$/ ha** |
| Jumla ya Mategemeo ya Ongezeko la Msitu kwa Mwaka (JMOMM) = WOM*EK $m^3$ | **6045.32** |
| Kiwango cha juu cha Uvunaji kwa Mwaka (KJUM)= JMOMM/5 (Kiwango cha juu 5,000 $m^3$) | **1209.06 $m^3$** |
| Wastani wa Ujazo wa Mti (WUM) $m^3$ | **2$m^3$** |
| Kiwango cha juu cha Mti cha Kuvuna kwa mwaka (KJMK)=KJUM/WUM $m^3$ | **604.53 miti** |

Kila zoezi la uvunaji wa magogo lazima kufuata mgao wa jamii ya miti na kiwango kidogo cha kikomo.

## 12: MABAKI YA MBAO ZILIZOPO

*(Sehemu yote hii itatumika kwa misitu mipya ya hifadhi ya kijiji.)*

Kabla ya kuanzishwa hifadhi ya misitu ya kijiji kulikuwa na uvunaji ndani ya msitu. Mara kwa mara wavunaji walikuwa wanachukua magogo mazuri na makubwa: kama wakivuna mti na kugundua hauna ubora ndani walikuwa wanauacha msituni pamoja na matawi. Uvunaji unaoendelea kwa sasa hautaruhusu uwepo wa mabaki hayo, lakini itakuwa vema kuwezesha uuzaji wa mabaki yaliyoachwa kwenye msitu. makadirio ya mabaki ya mbao yaliyopo kwenye msitu yatakayotumika kwa sasa ni kama ifuatavyo.

| **Jamii ya mti** | **Kiasi** | **Ukubwa wa vipande vya magogo vilivyopo** |
|---|---|---|

| **Jamii ya mti** | **Kiasi** | **Ukubwa wa vipande vya magogo vilivyopo** |
|---|---|---|
| Mninga | $50m^3$ | Mfano: magogo yenye mzunguko wa 40 sentimeta na urefu wa mita 1.5m |
| Mpangapanga | | |
| Mpingo | | |

## KIAMBATANISHO 1 : TATHMINI YA KUPATA KIASI CHA KUVUNA

1) Matembezi ya kukatisha msitu yalifanyika mara 10. Kila mstari wa kukatisha msitu ulikuwa na upana wa mita 10 na na urefu wa kilomita 96.43. Zoezi lilifanyika kati ya tarehe 11/2/2018 na tarehe 21/2/2018. Hivyo ukubwa wa eneo la matembezi ni kilomita za mraba 96.43.

2) Ili kuweza kupata kisio la kiasi cha miti kwa eneo lote la msitu, eneo la msitu kwa ujumla liligawanywa kwa jumla ya umbali wa matembezi ya mkato. Jibu lililopatikana linakuwa namba ya kuzidisha ambayo itatumika kupata makadirio ya idadi ya miti yote katika msitu.

| | |
|---|---|
| Jumla ya urefu wa matembezi ya mkato (MT) | 96.43 km |
| Eneo la kuvuna (EK) | 13142 ha |
| Namba ya kuzidisha Eneo NK = EK / MT | 136 |

3) Idadi ya miti iliyohesabiwa wakati wa tathmini imeorodheshwa kwa kila jamii ya miti.

| **Jumla ya Miti Iliyohesabiwa** | **MD** | **KT** | **MK** |
|---|---|---|---|
| Mpingo | 44 | 173 | 126 |
| Mpangapanga | 800 | 108 | 0 |
| Msenjele | 240 | 324 | 16 |
| Mlondondo | 144 | 198 | 1 |
| Mninga jangwa | 47 | 56 | 1 |
| Mkongo | 116 | 33 | 0 |
| Mkwaju | 53 | 81 | 2 |
| Mgongo | 42 | 110 | 0 |
| Mpupi | 121 | 27 | 0 |
| Msufi Pori | 20 | 39 | 3 |
| Mchenga | 61 | 42 | 2 |
| Mnidu | 10 | 23 | 2 |
| Mkunya | 46 | 62 | 8 |
| Mninga bonde | 0 | 12 | 8 |
| Mnepa | 126 | 13 | 0 |
| Mlipa deni | 5 | 27 | 0 |
| Mkuliungu | 76 | 4 | 0 |
| Mtumbitumbi | 9 | 7 | 1 |
| Mjuju | 42 | 4 | 0 |
| Mtanga | 2 | 8 | 2 |
| Mjembe | 19 | 3 | 0 |

4) Idadi ya Miti iliyoonyeshwa hapo chini ndiyo miti iliyokomaa kwa kuvuna. Ili kuweza kupata mgawo huo kimahesabu mambo muhimu yalizingatiwa kama vile muda ambao aina ya Mti huchukua kufikia umri wa kuvuna, idadi ya Miti itakayokufa / kuathirika kwa njia za Asilia kama Magonjwa, Ukame n.k pamoja na idadi ya miti iliyohesabiwa katika matembezi ya kukatisha msitu. Kwa ujumla mistari ya matembezi mkato ikiwa mirefu zaidi ndivyo matokeo kimahesabu yanakuwa mazuri zaidi.Vigezo hivi vimejumuishwa katika Jedwali la mgawo wa kuvuna. Kwa hiyo tunaweza kukadiria miti ya kuvuna katika matembezi ya kukatisha msitu kama ifuatavyo:

| **Kiwango cha Kuvunwa Kiendelevu** | **MKT** | **MMK** |
|---|---:|---:|
| Mpingo | 9.17 | 3.95 |
| Mpangapanga | 7.95 | 0.00 |
| Msenjele | 24.62 | 0.69 |
| Mlondondo | 15.43 | 0.00 |
| Mninga jangwa | 4.26 | 0.00 |
| Mkongo | 2.23 | 0.00 |
| Mkwaju | 6.31 | 0.00 |
| Mgongo | 8.78 | 0.00 |
| Mpupi | 1.83 | 0.00 |
| Msufi Pori | 2.64 | 0.00 |
| Mchenga | 3.04 | 0.00 |
| Mnidu | 1.44 | 0.00 |
| Mkunya | 4.67 | 0.31 |
| Mninga bonde | 0.81 | 0.31 |
| Mnepa | 0.81 | 0.00 |
| Mlipa deni | 1.83 | 0.00 |
| Mkuliungu | 0.00 | 0.00 |
| Mtumbitumbi | 0.43 | 0.00 |
| Mjuju | 0.00 | 0.00 |
| Mtanga | 0.51 | 0.00 |

5) Miti Midogo itakua na kuingia katika kundi la Miti ya kati na mikubwa na kama itakuwa haitoshi inabidi kupunguza kiasi cha mgawo ili tuweze kuendelea na uvunaji endelevu. Pia inakadiriwa kuwa kama theluthi moja (moja ya tatu) ya miti midogo inaweza kufa kabla ya kukua na kufikia kiwango cha miti ya kati. Hatua inayofuata ni ya kufanya marekebisho ya makisio kutokana na vigezo hapo juu;

| **Jamii ya mti** | **Mpingo** | **Mpangapanga** | **Msenjele** | **Mlondondo** | **Mninga jangwa** | **Mkongo** | **Mkwaju** | **Mgongo** | **Mpupi** | **Msufi Pori** | **Mchenga** | **Mnidu** | **Mkunya** | **Mninga bonde** | **Mnepa** | **Mlipadeni** | **Mtumbitumbi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Miti Midogo iliyofanyiwa marekebisho MD’ = MD x 2 / 3 | 29 | 533 | 160 | 96 | 31 | 77 | 35 | 28 | 80 | 13 | 40 | 6 | 30 | 0 | 84 | 3 | 6 |
| Jumla J1 = KT + MK | 29 | 533 | 160 | 96 | 31 | 33 | 83 | 110 | 27 | 42 | 44 | 25 | 70 | 20 | 13 | 27 | 8 |
| Jumla J2 = (MD’ + KT + MK) / 2 | 29 | 533 | 160 | 96 | 31 | 55 | 59 | 69 | 53.5 | 27.5 | 42 | 15.5 | 50 | 10 | 48.5 | 15 | 7 |
| Jumla J3 = Kiwango cha chini (J1, J2) | 29 | 533 | 160 | 96 | 31 | 33 | 59 | 69 | 27 | 27.5 | 42 | 15.5 | 50 | 10 | 13 | 15 | 7 |
| Rekebisho kwa miti | 29 | 533 | 160 | 96 | 31 | 1 | 0.711 | 0.627 | 1 | 0.655 | 0.955 | 0.62 | 0.714 | 0.5 | 1 | 0.556 | 0.875 |

| | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| mikubwa naya kijani NZM = J3 / J1 | | | | | | | | | | | | | | | | | |

6) Hatua ya mwisho ni kujumuisha takwimu zote hapo juu ili kupata mgawo wa ambao utatumika ili kuwa na uvunaji endelevu. Kiasi cha kuvuna kwa kila jamii ya Mti ni:

Mgao wa Uvunaji wa KT (Kijani) KKT = MKT × NZE × NZM

Mgao wa Uvunaji wa MK (bluu) KMK = MMK = KBT × NZE × NZM

Mgao wa mwisho kwa kila jamii ya mti kama ifuatavyo:

| **Kiasi cha Kuvuna Kiendelevu katika Msitu** | **KKT** | **KMK** | **Ujazo ($m^3$)** | **Ujazo kwa Mwaka ($m^3$)** |
|---|---:|---:|---:|---:|
| Mpingo | 684 | 295 | 912 | 182 |
| Mpangapanga | 1,083 | 0 | 1880 | 376 |
| Msenjele | 2,466 | 69 | 3375 | 675 |
| Mlondondo | 1,558 | 0 | 2141 | 428 |
| Mninga jangwa | 448 | 0 | 667 | 133 |
| Mkongo | 303 | 0 | 819 | 164 |
| Mkwaju | 611 | 0 | 1602 | 320 |
| Mgongo | 750 | 0 | 1788 | 358 |
| Mpupi | 249 | 0 | 458 | 92 |
| Msufi Pori | 235 | 0 | 742 | 148 |
| Mchenga | 395 | 0 | 620 | 124 |
| Mnidu | 121 | 0 | 255 | 51 |
| Mkunya | 454 | 30 | 1,693 | 339 |
| Mninga bonde | 55 | 21 | 220 | 44 |
| Mnepa | 110 | 0 | 201 | 40 |
| Mlipa deni | 138 | 0 | 242 | 48 |
| Mtumbitumbi | 51 | 0 | 171 | 34 |